KISWAHILI ACTIVITIES 5

KUSIKILIZA NA KUONGEA, KUSOMA KWA SAUTI

Sehemu ya A: Kusikiliza na kuongea

Ningependa tuzungumze kuhusu heshima na adabu. Wewe ni kiranja wa darasa lako una mazungumzo na mwalimu wako wa darasa.

1. Toa maelezo mafupi vile utakavyoonyesha heshima na adabu kwa mgeni aliyealikwa nyumbani kwenu.
   (Mwanafunzi ajibu)
2. Anza mazungumzo kwa maamkizi yafuatayo.
   (Mwanafunzi ajibu)
3. Taja maneno ya adabu ambayo kama kiranja unawasisitizia wanafunzi kuyatumia darasani.
   (Mwanafunzi ajibu)
4. Eleza mwalimu umuhimu wa kuwa mwanafunzi mwenye heshima na adabu.
   (Mwanafunzi ajibu)
5. Taja maneno ya heshima na adabu badala ya maneno uliyopewa
   a. Mtoto anahara _____
   b. Fatuma ana mimba _____
   c. Halima amezaa _____

Sehemu ya B: Kusoma Kwa Sauti

Mama alikumbuka kuwa baba alisahau kumeza dawa. Aliingia chumbani na kutoka na vidonge viwili vya dawa akampa baba aweze kumeza kwa maji. Baba alikuwa na ugonjwa wa kisukari na shinikizo la damu.

Alikuwa anatueleza kuwa ugonjwa wake ulitokana na hali ya maisha katika harakati zake za biashara ambayo ilikuwa mara inapanda mara inashuka. Alikuwa akizinunua bidhaa kutoka Uchina na kuziuza humu nchini. Ingawa aliipenda biashara hiyo, aliichukia hali ile ya ugonjwa na hivyo akaamua kupunguza shughuli zake na kuongeza muda wa kupumzika nasi nyumbani.

Baba alipokata kauli kupunguza shughuli aliendelea kuwa na afya nzuri. Tuliendelea kuzungumza naye mambo aliyofurahia kusikiliza kama vile umilisi tuliokuwa tumepata shuleni. Hasa, alifurahi tulipomwambia tulijifunza kuhusu jinsi ya kuzuia magonjwa. Tulimweleza pia kuhusu magonjwa yanayotokana na hali za maisha kama vile kisukari na shinikizo la damu.

SEHEMU YA A: Ufahamu